Aina Tatu Za Ibada

na

Ellis Forsman

Aina Tatu Za Ibada

na

Ellis Forsman

Octoba 15, 2011

Aina Tatu Za Ibada

Yoh. 4:21-24

Kiasili mwanadamu ni kiumbe kinachoabudu. Popote alipotengeneza historia amekuwa akiabudu kitu.

Katika kila nchi, katika kila enzi, akiwa na Biblia au hana, iwe ameishi juu ya nchi kumekuwa na asili ndani yake wazo la ibada.

Biblia inatuambia ni nani na jinsi ya kuabudu.

Neno "ibada" inapatikana mara 190 katika Biblia.

- Mat. 4:10, "*Ndipo Yesu alipomwambia nenda zako shetani, kwa maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye pekee yake.*"
- Ufu. 22:8-9, "*Nami Yohana ndimi niliyeyasikia na kuyaona mambo hayo. Na hapo nilipoyasikia na kuyaona nalianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule mwenye kunionyesha hayo. Naye akaniambia, angalia usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu.*"

Katika vifungu hivi tunaagizwa kwamba tumwabudu Mungu.

- Hatuombi kwa malaika.
- Hatuombi kwa Mariamu, mama wa Yesu, kama wakatholiki wanavyofanya.
- Hatuombi pia kwa Yesu, bali tunapaswa kuomba kupitia kwake hadi kwa Mungu. Yesu ni mpatanishi wetu.
- 1 Tim. 2:5, "*Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu;*"
- Yoh. 16:23-24, "*Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amini, amini, nawaambia, mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.*"

Kuna aina tatu za ibada zilizotajwa katika Agano Jipya.

Ibada ya bure. Mat. 15:9, "*Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*"

Ibada ya kijinga. Mdo. 17:23, "*Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubiri habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua.*"

Ibada ya kweli. Yoh. 4:21-24, "*Yesu akamwambia mama unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalemu. Ninyi manaabudu msichokijua sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi. Lakini saa inakuja nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wa mwabudu. Mungu ni Roho nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Ibada ya bure

Wayahudi walikuwa na kitu cha kweli cha kuabudu (Mungu), lakini ibada yao ilikuwa bure.

- Mat. 15:2-3, "*Mbona wanafunzi wako huyaalifu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula. Akajibu akawaambia mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?*"
- Mat. 15:8-9, "*Naye Yesu akafahamu, akawaambia mbona mnabishana ninyi kwa ninyi, enyi wa imani chache, kwa sababu hamna mikate? Hamjafahamu bado, wala hamkumbuki ile mikate mitano kwa wale elfu tano, na vikapu vingapi mlivyo viokota?*"

Swali ambalo Waandishi na Mafarisayo walimwuliza Yesu:

Mat. 15:2, "*Mbona wanafunzi wako huyaalifu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula.*"

"*Mapokeo ya wazee*" humaanisha mila za dini au desturi ambazo zilitolewa kwa kizazi hadi kizazi miongoni mwa Wayahudi, na ikaandikwa katika Talmud.

Mapokeo haya yalichukuliwa kuwa sawa katika ulinganifu wa Sheria ya Musa.

Mapokeo haya yalishinikizwa miongoni mwa Wayahudi, na adhabu ilitolewa kwa mtu aliyevunja Sheria ya Musa.

Mafarisayo wakaona kwamba wanafunzi wa Yesu hawakuosha mikono walipokua wakila mikate. Sheria yao katika Talmud ilisema, "atakaye kula mkate bila kuosha mikono ni mchafu kana kwamba amefanya uzinzi."

Lakini Yesu anaonyesha utofauti kati ya desturi zao na neno la Mungu, na akajibu swali lao kwa kuuliza, "Kwa nini nanyi uihalifu amri ya Mungu kwa mapokeo yenu?" (mustari wa 3).

Hivyo, Yesu alionyesha kwamba neno la Mungu lishikiliwe kwa dhati zaidi ya mambo yote. Mapokeo yao yalikuwa ni maneno ya wanadamu, lakini sheria ya Musa ilikuwa neno la Mungu.

Kwa vile, Yesu anasema kwamba ibada yao ni bure.

Mat. 15:8-9, "*Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali anmi, nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*"

"*Bure*" humaanisha "tupu, haina faida, haina matunda, haina cho chote, isiyo na maana au ubora."

Ibada yao ilikuwaje bure? Walizidisha mapokeo ya wanadamu kwa maagizo ya Mungu.

Kuoshwa mikono iliagizwa, na haikudhuru upande wo wote katika maagizo ya Mungu, hiyo ni, hadi walipoiongeza kuwa sheria; hapo ikawa ibada ya bure.

Kuongeza katika neno la Mungu ilikuwa ni makusudi kwao.

Petro naye alikuwa na makusudi pale alipofikiria wazo la kuabudu kwa njia yake.

Mat. 17:1-5, "*Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani; akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Na tazama wakatokewa na Musa na Eliya, wakizungumza naye. Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema tazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye; msikieni yeye.*"

Kwa vile, kila tendo ambacho wanadamu wanafanya kama ibada Mungu hajaagiza, hiyo inakuwa ibada ya "bure".

Mifano michache ya kisasa (ibada):

- Kuhesabu lozari.
- Ubatizo wa watoto wachanga.
- Vyombo vya mziki katika ibada.

Nabii Isaya akizungumzia ufalme wa Kristo:

Isa. 28:16-17, "*Kwa ajili ya hayo Bwana MUNGU asema hivi, tazama naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka. Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni, na haki kuwa ndiyo timazi; na mvua yam awe itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo, na maji yatapagharikisha mahali pa kujisitiri.*"

Ibada ya kijinga

Paulo akiongea juu ya Milima Mengi huko Athene.

- Mdo. 17:23-27, "*Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubiri habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojegwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote, kwa maana ndiye anyewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wan chi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa papasa, wakamwone ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu.*"
- Mdo. 17:30-31, "*Basi zamani zile za ujinga, Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.*"

"*Naliona mahali iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA.*" (mustari 23).

Waathene waliweka minara kwa miungu tofauti walioamini kwamba ilikuwepo; vitu hivi waliviabudu. Lakini kuhakikisha hawakuacha

mungu ye yote nje ya ibada yao ambayo hawakugundua, wakaweka tena nyingine KWA MUNGU ASIYEJULIKANA.

Paulo sasa anapendekeza awafahamishe kuhusu Mungu huyu asiyejulikana. Kwa vile walitambua ukengeufu wao dhidi ya Mungu huyu, angeweza kuwaambia ukweli kumhusu Yeye.

Wakati fulani Paulo akatoa tabia ya kweli na asili ya Mungu huyu, iliyo mtofautisha na miungu mingine.

Mungu huyu "*alifanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo*."

Hii ilijulikana hata miongoni mwa wanafalsafa, lakini wale waliotoka katika shule ya Aristotle waliikataa, na wakabaki kwamba "ulimwengu ulianzia umilele, na kila kitu kilikuwa kama kilivyo sasa."

Mungu huyu, "*hakai katika hekalu zilizofanywa kwa mikono*"

Hekalu zilizofanywa kwa mikono hashikamani navyo.

Kama hata hekalu la Sulemani, iliyowekwa kwa ajili ya kumwabudia Mungu wa Israeli, hakuweza kushikamana nacho, iweje vitu vya ajabu vya Waathene, iliyotolewa kwa miungu ambayo haikuwa miungu?

1 Fal. 8:27, "*Lakini Mungu je atakaa kweli kweli juu ya nchi? Tazama mbingu hazikutoshi, wala mbingu za mbingu; sembuse nyumba hii niliyoijenga!*"

Mungu huyu "*haabudiwi kwa mikono ya wanadamu.*"

Mungu huyu hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu hata kama anaitaji cho chote ambacho yanaweza kusaidia, tukiona hilo kutoka kwake wanadamu wakapata uzima na pumzi na vitu vyote.

Mungu aliyeufanya ulimwengu ataihukumu.

Mdo. 17:30-31, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku ambayo atawahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.*"

Wakati fulani Mungu aliruhusu mataifa watembee katika ukengeufu na kuonyesha kile wanadamu wanaweza kufanya, na kulikuwa na umuhimu kiasi gani la ufunuo kuwaagiza katika ujuzi wa kweli wa Mungu.

Hatutakiwi kudhani kwamba Mungu alichukua ibada ya sanamu kuwa ni wema au uhalifu na silaha ambazo ibada ya sanamu huongoza pasipo umuhimu, lakini aliteska ili kwamba nchi hizo waishi pasipo kuwa na hukumu ya moja kwa moja dhidi yao. Lakini mwisho wa ulimwengu, watu wote watakuja mbele zake katika hukumu.

2 Kor. 5:10, "*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda kwamba ni mema au mabaya.*"

Ibada ya kweli

Yoh. 4:21-24, "*Yesu akamwambia mama unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalemu. Ninyi mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wikovu watoka kwa Wayahudi. Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo hali watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Kipindi kilichopita, kumwabudu Mungu ulifanyika mahali pamoja.

Wasamaria walimwabudu "*katika mlima*" (msitari 21), huo ni mlima Gerasi.

Wayahudi walimwabudu "*Yerusalemu*". (msitari 21).

Lakini sasa, Mungu hapaswi kuabudiwa sehemu moja (msitari 23).

Mungu anapaswa kuabudiwa "*katika roho na katika kweli*" (msitari 24).

Hapa Yesu anaonyesha mambo matatu ya ibada ya kweli.

Mungu ndiye anafaa kuwa mlengwa wa ibada yetu.

- Mat. 4:10, "*Ndipo Yesu alipomwambia, nenda zako shetani, kwa maana imeandika msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye pekee yake.*"
- Ufu. 22:8-9, "*Nami Yohana ndimi niliyeyasikia na kuyaona mambo hayo. Na hapo nilipoyasikia na kuyaona nalianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule mwenye kunionyesha hayo. Naye akaniambia, angalia usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu.*"

Kuabudu "*katika roho*" – Nia njema au dhamira ya ibada yetu. Ibada lazima ifanyike kwa nia njema na hamu njema ili kukidhi uthibitisho wa mbinguni.

Kuabudu "*katika kweli*" – njia sahihi ya kuabudu.

Yoh. 17:17, "*Uwatakase na kweli yako; neno lako ndiyo kweli.*"

Mambo matano yote lazima yawe katika ibada zetu leo. Tunaweza kufanya jaribio katika mambo yote ya ibada zetu:

- Sala.
- Kuimba.
- Kuhubiri.
- Changizo.
- Meza ya Bwana.

Hitimisho

Hebu na tuakikishe kwamba ibada yetu mara zote ni safi na ipo kimaandiko.

Hebu tuangalie kwamba ibada yetu siyo hasara; hiyo ni kwamba sio ibada ya kijinga; na kwamba ni ibada ya kweli katika mtiririko wa Agano Jipya.